



**OFISI YA MKUU WA
WILAYA YA SHINYANGA.**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UJIO WA MWENGE WA UHURU
KWA MWAKA 2024**

Shinyanga

09 Agosti 2024

Wilaya ya Shinyanga inatarajia kupokea na kukimbiza Mwenge wa Uhuru kwa siku mbili Agosti 11 na 12, 2024 katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ukitokea Wilaya ya Kishapu na baada ya hapo utakabidhiwa Wilaya ya Kahama. Mwenge utakimbizwa umbali wa kilometa 234.5 kiwilaya na utazindua, kuweka mawe ya msingi na kukagua jumla ya miradi 24 yenye thamani ya shilingi 6,075,929,357 (6.07 Bil). Miradi ya maendeleo itakayotembelewa itahusisha elimu, afya, mazingira, miundombinu, uchaguzi, maendeleo ya jamii n.k.

Mwenge utawasili katika Wilaya ya Shinyanga na kupokelewa na wakazi wa Manispaa ya Shinyanga siku ya Jumapili 11 Agosti 2024, saa 12 asubuhi katika eneo la uwanja wa Shule ya Msingi Ibadakuli "A". Baada ya mapokezi, Mwenge wa Uhuru utakimbizwa umbali wa kilometa 74.5 kwa kutembelea jumla ya miradi ya maendeleo 10 yenye thamani ya shilingi 4,287,605,662 (4.2 Bil), na utakesha katika viwanja vya Sabasaba, Manispaa ya Wilaya ya Shinyanga.

Wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga wataupokea Mwenge wa Uhuru siku ya Jumatatu Agosti 12, 2024, saa 12 Asubuni katika eneo la uwanja wa michezo Mwalukwa kata ya Mwalukwa. Mwenge wa Uhuru utakimbizwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kwa umbali wa kilometa 160 na kutembelea jumla ya miradi 14 yenye thamani ya Shilingi 1,788,323,695 (1.7 Bil).

Mwenge wa Uhuru pia utahamasisha shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu. Uhamasishaji huo utafanyika chini ya kauli mbiu ya Mwenge wa Uhuru 2024 “Tunza Mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu”

Aidha, katika maeneo ya mkesha, shamrashamra za mwenge zitaambatana na shughuli mbalimbali za kijamii zikiwemo makongamano ya vijana, utoaji wa elimu ya uchaguzi wa serikali za mitaa, upimaji wa afya ikihusisha upimaji wa virusi vya UKIMWI, malaria na magonjwa mengine. Vikundi mbalimbali vya hamasa na burudani vitasherehesha mbio za mwenge wa Uhuru wakiwemo wasanii wa kitaifa. Hivyo, natoa rai kwa wananchi wote kushiriki kikamilifu kwa kujitokeza maeneo yote Mwenge wa Uhuru utakapopokelewa, utakakopita na kukesha kwa kuushangilia.

Mbio za Mwenge wa Uhuru hufanyika kila Mwaka. Mwenge wa uhuru ni mojawapo ya alama za taifa unashiria uhuru na mwanga ambao uliwashwa na kunyanyuliwa katika kilele cha Mlima Kilimanjaro mnamo Desemba, 1961.

Imetolewa na:

Adv. Julius S. Mtatiro

MKUU WA WILAYA YA SHINYANGA